

TAARIFA KWA UMMA

MRADI WA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA YA NCHI KATIKA MKOA WA SIMIYU

**Yah: UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA UTHAMINI WA MALI NA ARDHI KATIKA
ENE LA MRADI –AWAMU YA KWANZA BUSEGA, BARIADI NA ITILIMA**

Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) iliwasilisha ombi la kupatiwa fedha toka Mfuko wa Kimataifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Fund*) (*GCF*) ili kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Mkoa wa Simiyu ikiwa ni mkakati wa Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi (*Simiyu Climate Resilient Water Supply Project*). Mradi huu utatekelezwa katika Wilaya tano za Mkoa wa Simiyu ambazo ni Busega, Bariadi, Itilima, Maswa na Meatu na utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu utajumuisha Wilaya za Busega, Itilima na Bariadi kwa muda wa miaka mitano. Gharama za mradi zitachangiwa kwa pamoja kutoka Serikali ya Tanzania na Wadau wa Maendeleo. Kulingana na mkataba wa makubaliano ya utoaji fedha (*Financing agreement*), *GCF* watachangia *EURO Milioni 102.7*, Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika Benk ya Maendeleo ya Ujerumani itachangia *EURO Milioni 26.1* na Serikali ya Tanzania *EURO Milioni 40.7* na Wananchi kupitia nguvu zao (*in kind contribution*) watachangia *EURO Milioni 1.5*. Aidha, mradi huu utakuwa maeneo makuu manne ya utekelezaji ambayo ni; Uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, uanzishaji wa kilimo himilivu dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi (*Climate Smart Agriculture*), ujenzi wa mabwawa madogo madogo ya umwagiliaji na kujenga uwezo katika usimamiaji wa mradi.

Serikali imeanza taratibu za kufanya uthamini wa mali na ardhi kwa wananchi wote watakaotakiwa kupisha ujenzi wa miundombinu ya mradi itakayojumuisha ujenzi wa njia ya bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima lenye urefu wa kilometa 167. Kwa kuwa gharama za utekelezaji wa mradi unajumuisha ufadhili kutoka taasisi za kimataifa, taarifa ni hatua muhimu ya kuwajulisha Wananchi kabla ya kuanza rasmi zoezi la uthamini. Uthamini utafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi No. 4 ya Mwaka 1999, Sheria ya Uthamini Na.7 ya Mwaka 2016 na Sheria ya Utwaaji wa Ardhi No. 47 ya mwaka 1967 pamoja na miongozo yake.

Kwa taarifa hii Serikali inawajulisha Wananchi wote ambao maeneo yao yatapitiwa na mradi kuwa, kazi ya uhamasishaji na hatimaye uthamini itaanza kuanzia tarehe 16 Novemba, 2019.



Mhe. Anthony J. Mtaka

MKUU WA MKOA WA SIMIYU

01 Novemba, 2019